

III: MAMBO YA MSINGI KATIKA UTUNZAJI WA PAKA.

- Paka ni wanyama wenye kujitawala, wasafi, wakipewa uangalifu wa kawaida wanaoweza kujitunza wenyewe.
- Paka wanaoweza kula nyama, mabaki ya nyama, kuku, samaki, mabaki ya mezani/chakula, maziwa, mayai, wali na chakula kitokanacho na mahindi.
- Paka wakubwa lazima wapewe mlo mmoja au zaidi, pia chakula kiwepo wakati wote.
- Paka ni wala nyama kwa kiasi kikubwa, lakini anaweza kula mpaka 50% ya wanga kama atachanganyiwa kwenye nyama.
- Paka hawahitaji sehemu maalumu ya kulala, huweza kupata sehemu nzuri wao wenyewe ndani ya nyumba.
- Paka wanahitaji chanjo dhidi ya kichaa kila mwaka kwa usalama wao na watu walio karibu nao, wanatakiwa wachanjwe dhidi ya mafua ya paka katika wakati mmoja kama unauwezo.
- Paka wapatiwe dawa ya minyoo mara kwa mara (kila baada ya miezi mitatu), hasa kama ni wawindaji, kwani huweza kupata minyoo kwa njia hii.
- Paka wachunguzwe wadudu mara kwa mara. Kama wanaviroboto na kupe wachache unaweza kuwatoa. Kama paka wanakupe na viroboto wengi wapelekwe kwa mtaalamu wa mifugo.
- Paka huzaliana kwa haraka, kama inawezekana ni vizuri kumtoa viungo vya uzazi, hii hufanywa na daktari wa mifugo. Hii huwafanya waishi maisha marefu na yenye furaha.

KUMBUKA: DAIMA KUWA MWEMA KWA PAKA.

IMEFADHILIWA NA:

Naturewatch Foundation
For the advancement of animal welfare



OCTOBER 4

Tanzania Animal Welfare Society

AWESO

P.O. Box 10268, Dar es Salaam, Tanzania

Tel: +255 713 322796 /+255 752 660 101/ +255 715 447005

E-mail: tzanimal@yahoo.com, info@taweso.org

Website: www.taweso.org

SIKU YA WANYAMA DUNIANI, OCTOBA-2015 I: MAMBO YA MSINGI KATIKA UTUNZAJI WA PUNDA

- Punda ni jamii ya wanyama walao majani, Punda hupendelea zaidi nyasi kama chanzo chao cha chakula, lakini huzoea vizuri chakula cha ziada chenye uwiano mzuri wa nishati na kambakamba. Ni muhimu kukumbuka kwamba chakula chenye ubora wa juu kitakuwa na utendaji mzuri zaidi. Punda apewe mlo miwili kwa siku/katika masaa 24.
- Maji ni muhimu/lazima kwa punda, maji ni muhimu yawepo wakati wote ambao punda hafanyi kazi.
- Punda apatiwe banda linalofaa wakati ambao hafanyi kazi na nyakati za usiku. Banda lazima liwe na kivuli na linaloweza kumkinga dhidi ya upepo na mvua, ili aendelee kuwa na afya nzuri.
- Punda mwenye mimba yenye miezi zaidi ya minane haitakiwi afanyishwe kazi, na baada ya kuzaa ni miezi mitatu ndipo punda aanze kufanya kazi.
- Tafuta/omba ushauri wa mtaalamu wa mifugo kuhusu chanjo za punda, chanjo ya kichaa cha mbwa hutolewa mara moja kwa mwaka. Ni muhimu dawa za minyoo zitolewe mara kwa mara, hili linaweza kufanywa na mfugaji mwenyewe.
- Miguu ya punda wafanyao kazi inatakiwa itunzwe vizuri kwani ni muhimu katika utendaji wao wa kazi. Ni muhimu ikaguliwe mara kwa mara na kutibiwa inapohitajika.

- Punda wakotao miokotoni lazima wavalishwe hatamu/mira inayofaa na yenye kinga ambayo haiwezi kuumiza uti wa mgongo au kukata ngozi ya punda.
- Punda walio chini ya umri wa miaka mitano wasibebebweshwe mizigo au kuvuta waliokotoni. Kwani mifupa yao ni laini kabla ya umri huo(miaka mitatu). Kama watafanyishwa kazi mapema wanaweza kuvunjika miguu na migongo, na kusababisha mateso na kufupisha uhai na maisha yao ya kufanya kazi kwa ujumla.
- Kamwe Punda wasibebebweshwe mizigo kupita kiasi. Kwanza ni ukatili wa hali ya juu, lakini pia inapunguza muda wake wa maisha ya kufanya kazi. Punda wanaobebeba mizigo kupita kiasi hufa na umri wa miaka 10, tofauti na punda wenye afya ambao huishi miaka 20 zaidi.
- Kuhusu ubebebweshaji wa mizigo kupita kiasi: Punda mdogo (mwenye urefu wa sentimita 102 mabegani) yafaa abebe mizigo usiozidi kilo 50, Punda mwenye saizi ya kati(102-112) kilo 63 na Punda mkubwa (zaidi ya 112) kilo 76.
- Mwisho upigaji wa Punda ni ukatili na usio wa lazima na huonesha uwezo mbovu wa dereva, na pia inaweza ikasababisha kushitakiwa kwa makosa ya jinai.

KUMBUKA: DAIMA SIKU ZOTE KUWA MWEEMA KWA PUNDA

II: MAMBO YA MSINGI KATIKA UTUNZAJI WA MBWA

- Mbwa hula vyakula tofauti, Mbwa huweza kula vyakula vingi ambavyo huliwa na binadamu. Mlo kamili kwa mbwa unajumuisha protini kama vile nyama, matumbo, kuku, mayai na maharagwe. Mbwa pia huhitaji vyakula vya wanga kama vile mahindi, mchele au vyakula vya mbwa viuzavyo. Mbogamboga kama vile karoti, kabeji au spinachi ni vyanzo vizuri vya vitamini na vyakula ghafi/vyakula vigumu.
- Mbwa mkubwa anahitaji mlo mmoja kwa siku.
- Mbwa wadogo wanahitaji mlo mitatu kwa ukuaji mzuri.
- Mbwa anahitaji maji safi ya kunywa wakati wote.
- Mbwa anahitaji makazi mazuri yatakayomkinga na mvua na jua na pia yenye hewa ya kutosha. Kama inawezekana mbwa asifungiwe ndani, ili kuzuia mbwa asizurure weka uzio kuzunguka banda la mbwa.
- Mbwa lazima wachanjwe dhidi ya kichaa cha mbwa KILA MWAKA! hii ni sheria. Kama unaweza kumudu gharama wapatie pia chanjo dhidi ya distempa, homa ya manjano, leptosporosi na magonjwa mengine.
- Uogeshaji wa mbwa mara moja kwa wiki husaidia kuwakinga wasipatwe na kupe na viroboto. Ni vizuri zaidi kutumia dawa dhidi ya wadudu, soma maelekezo kwa makini kabla ya kutumia dawa hizo.
- Mbwa wapatiwe dawa za minyoo kila baada ya miezi mitatu(hakikisha unatumia dawa ya minyoo ya kutosha).
- Mbwa wanahitaji mazoezi ya mara kwa mara/kila siku.
- Mbwa anaauwezo wa kuzaa kila baada ya miezi sita, japokuwa hii haishauriwi kwani humdhoofisha mbwa, mara moja kwa mwaka ni vizuri. Ni vizuri kumhasi/kumtoa kizazi mbwa ili kuepuka watoto wasiotakiwa, hii hufanywa na daktari wa wanyama, na kama unahitaji msaaada wasiliana na kiongozi SPCA wa eneo lako au kikundi cha ustawi wa jamii/haki za wanyama.

KUMBUKA: DAIMA SIKU ZOTE KUWA MWEEMA KWA MBWA.